

Maswali

1. Mfalme aliamrisha Vashti afanye nini?
2. Vashti alisema nini?
3. Kwa vile Mfalme hakutaka kumuona Vashti tena, Alifanya nini?
4. Nani alichaguliwa kama Malkia mpya?
5. Nani alikuwa rafiki wa Mfalme?
6. Mbona Hamani alimchukia Mordekai?
7. Hamani alipanga kufanya nini?
8. Esta alimwambia nani?
9. Nani alinyongewa kwa mti wake mwenyewe?
10. Nani alifanywa mtu wa maana badala ya Hamani?

Majibu

1. Vashti aliamriwa kuja kwa Mfalme hali amevaa taji
2. Vashti alikataa
3. Mfalme alichagua Malkia mwingine
4. Esta alichaguliwa kama Malkia mpya
5. Rafiki alikuwa Hamani
6. Hamani alimchukia Mordekai kwa kukataa kumsujudia
7. Hamani alipanga kuwauwa wayahudi wote
8. Esta alimwambia Mfalme
9. Hamani alinyongewa kwa mti wake mwenyewe
10. Mordekai alifanywa kuwa wa maana badala ya Hamani

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 1



33 Malkia Esta

Marejeo

Esta

Kiini cha somo

Kuonyesha Mungu analinda watu wake

Maneno maalum

1. Karamu ya Mfalme + Nyumba ya mfalme + Vashti + hakuenda
2. Malkia + Mordekai + Myahudi + Esta
3. Rafiki + Hamani + chuki
4. Esta + ona Mfalme + maisha + ua + Wayahudi
5. Mfalme + kasirika + miti ya kunyongea + nyonga

33.1 Mfalme wa Uajemi alifanya karamu ya watu wakuu wa ufalme wake. Watumishi waliwekea wageni divai kwa vikombe vya dhahabu. Mfalme alipokuwa amekunywa zaidi, alitaka kuonyesha wageni urembo wa malkia wake. Alisema, “Ita malkia Vashti aje na awe amevaa taji ya fahari kwa kichwa chake.” Malkia Vashti hakuenda kwa sababu naye alikuwa ameandaa wanawake wa kifalme karamu ingine. Mfalme alikasirika sana na akauliza, “Tufanye je Vashti?” Watumishi wakamjibu, “Asikubaliwe kumuona Mfalme tena, na Mfalme achaguwe malkia mwingine badala ya Vashti.”

33.2 Mfalme alituma barua iende kwa ufalme wake wote ili wamtafutie wasichana warembo na wampelekee kwa nyumba ya kifalme. Mordekai myahudi alikuwa na mtoto wa mjomba aitwae Esta, aliyekuwa mzuri sana. Esta alipelekwa kwa nyumba ya kifalme. Waliingia mbele ya Mfalme mmoja baada ya mwingine. Mfalme alipomuona Esta alimpenda kuliko wengine. Alimvisha taji ya kifahari kwa kichwa na kumfanya malkia badala ya Vashti. Mfalme alimfanyia Malkia mpya karamu kubwa, karamu ya Esta.

Esta hakukuwa ameambia mtu yeyote kwamba alikuwa myahudi. Mordekai alikuwa amemkataza.



33.3 Mfalme alikuwa na rafiki yake Hamani na kila mtu alimsujudia. Mordekai alikataa kumsujudia naye Hamani akadhabika sana. Mordekai alikuwa amewaambia watumishi wa mfalme kwamba alikuwa myahudi, nao wakamwambia Hamani aliyemchukia Mordekai na wayahudi wote. Hamani alimwambia Mfalme juu ya watu waliokuwa wakiasi sheria yake. Akasema, “Nikuangamizie.” Mfalme alikubali.

Hamani alituma barua ili watu wawauwe wayahudi wote siku ya 13 mwezi wa kumi na mbili. Mordekai alipoona barua alilia na kuhuzunika sana.

33.4 Alimwambia malkia Esta naye akavaa mavazi ya Kifahari na kuenda na Mfalme alipokuwa amekaa Kwa kiti cha enzi. Mfalmealimuuliza, “Ni nini haja yako Malkia Esta? Nitakupa chochote hata nusu ya ufalme wangu.”

Esta akaalika mfalme na Hamani waende kwa karamu Pamoja naye. Kwa hivyo Walienda. Mfalme tena akauliza, “Unataka nini Malkia Esta?” “Oh! Mfalme, nipe uhai wangu pamoja na uhai wa watu wangu Wayahudi kwa sababu tunaenda kuuwawa wote.”

33.5 Mfalme alikasirika na kuuliza “Ni nani? Ni nani amethubutu kutenda hayo?” Esta alijibi, “Ni huyu Hamani mwovu”

Hamani alikuwa amejenga mti wa kunyongea Mordekai. Mfalme alisema “Nyongea Hamani mwenyewe.” Kwa hivyo wakamnyonga Hamani kwa huo mti aliounjenga Mordekai.

Mfalme akamfanya Mordekai mtu wa maana sana katika ufalme wake. Akawaandikia Wayahudi barua wawauwe adui wao wote. Mfalme aliwasaidia wayahudi kuwauwa adui wao wote.